

Scanned with CamScanner

# Does your absence from work matter?

**BY WALE AKINYEMI**
@waleakinyemi
wale@powertalks.biz

Have you ever tried to measure your value as a person? The fact that you are present does not mean you are valuable. Value is determined not by being present but by making your presence positively significant.

This is the game changer. If your presence in an organisation does not amount to positive significance, then you are not only a waste of space but an obstruction.

It means you are seated in the space where someone else could have sat and made positive significance.

Every agent of mediocrity is an obstruction to agents of transformation.

Every organisation has two kinds of people: the value adders and the parasites. Parasites do not add value but live off the value added by others. Yet they are always the first to complain about what is not working!

What determines your significance in the workplace is a personal choice. No one can do it for you.

The first question that needs to come to mind in determining the value that you add at work is to ask yourself the effect of your not being there.



> If your presence in an organisation does not add value, then you are not only a waste of space but an obstruction

Author and speaker Robin Sharma wrote a book with an interesting title; *When you die who will cry?* Quite frankly, there is no point in dying if you never lived. The fact that you breathe does not mean you live. That you move around does not mean you are progressing. That you are making noise does not mean you are being heard. Life is measured by impact and not by being present.

You need to have your trademark signature on everything you do. In essence, you may do what everyone does but you do it in a way that no one else does it. This becomes your signature. It is what people will remember.

The thing to differentiate you from the masses is your uniqueness. Ironically, uniqueness is one of the greatest things that have been fought by many and indeed by society. Yet when it thrives, it is claimed and celebrated.

No one wants to be different. Everyone wants to take solace in the fact that it was once done like this by someone else. Everyone wants to hide behind the uniqueness of others. The difference between an ordinary stone and a precious one is rarity. Value is always tied to uniqueness.

I cannot but talk about this wonderful staff of Kenya Airways that I once met at the airport. It was one of those days when the traffic on Mombasa road was hellish. I got to the airport late.

Unlike the ordinary treatment where the person at the counter would give a lecture on how you were supposed to be at the airport an hour before and all that, this one spared me. She empathized and made me relax and then went out of her way to help me. She differentiated herself by her uniqueness.

Uniqueness is not hard to come by. The problem is that we have copied people so much that we have forgotten our true identity. When mediocrity becomes so entrenched to the point of being cultural, then creativity will appear to be the odd one out. Remember, in a world dominated by fools, the wise appear to the majority as the fools.

You can find your true self again. The value that you may bring – just like that wonderful airline staff, may be a smile to brighten up someone's frustrating day. By her unique smile and sense of service, the ground hostess added value. She was not just present. Her presence was positively significant.

The next time I travel, if she is not there and the person who attends to me does not add value, I will truly miss that lady. When absence is unfelt, presence was unnecessary.

Your absence will either create a vacuum or cause joy. If it creates joy, then your presence was merely tolerated and not celebrated.

Have a positively significant weekend.

Scanned with CamScanner

April 12, 2021



NIPASHE UK 7

# RC apiga marufuku watoto wa kike kuchunga mifugo

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, amepiga marufuku watoto wa kike kwenda kuchunga mifugo, ili kuwaepusha na vishawishi vya kufanya ngono na kupata mimba za utotoni, hatua ambayo itawasababishia kukatisha masomo yao.

Telack alitangaza marufuku hiyo juzi kwenye kikao cha majadiliano cha kutokomeza mimba na ndoa za utotoni, kilicho andaliwa na Shirika la Msichana Initiative ambalo linatetea haki za watoto.

Alisema moja ya changamoto zinazochochea mimba za utotoni mkoani humo, ni watoto wa kike kwenda kuchunga mifugo maporini, hatua ambayo inawapa mwanya wa kukutana na wanaume na kisha kujamiiana na kuambulia ujauzito.

"Nawasihi wazazi na walezi mkoani Shinyanga, achaneni kabisa na tabia ya kupeleka watoto wa kike kwenda kuchunga mifugo, bali kazi hiyo ifanywe na wanaume ili kuwalinda dhidi ya mimba za utotoni na kutozima ndoto zao," alisema Telack.

Aidha, alisema kwa takwimu za utafiti zilizofanywa na Shirika la maendeleo ya watu na afya (TDHS) 2010, Mkoa wa Shinyanga ulitajwa kuongoza kwa mimba na ndoa za utotoni asilimia kwa 59, lakini kwa sasa wameshapiga hatua kubwa kuzipunguza, huku wakiendelea na mikakati ya kuhakikisha matukio hayo yanabaki kuwa historia.

Naye Mbunge wa Nkasi Kaskazini, Aida Kenani, akizungumza kwenye kikao hicho, alisema kuna haja kwa wadau na Serikali kuunganisha nguvu ya pamoja kutokomeza mimba na ndoa za utotoni, ikiwamo kuifanyia marekebisho ya haraka Sheria ya ndoa ya Mwaka 1971 ambayo ni kandamizi.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Shirika la Msichana Initiative, Rebeka Gyumi, alisema bado kuna kazi kubwa ya kuhakikisha tatizo hilo linakoma kabisa nchini, pamoja na kila mkoa kuweka mikakati yake namna watakavyo pambana kukomesha mimba na ndoa za utotoni, kama walivyofanya Mkoa wa Shinyanga.

HABARI LEO UK 17

# *Serikali kujenga vituo 40 mafunzo ufugaji samaki*

**Na Edward Kondela**

BALOZI wa Uholanzi nchini Tanzania, Jeroen Verheu amesema nchi yake iko tayari kusaidia ujenzi wa vituo vya mafunzo ya ufugaji samaki kuunga mkono mkakati wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kutoa mafunzo hayo kila wilaya.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mashimba Ndaki aliyasema hayo baada ya kuzungumza na Balozi Verheu katika ofisi ndogo za wizara jijini Dar es Salaam.

Alisema Balozi Verheu ameridhishwa na mkakati wa wizara na kwamba katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/22, wizara imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo 40 vya mafunzo ya ufugaji samaki.

"Sisi kama wizara tumeanza na mkakati huo na tumetenga fedha kwa ajili ya vituo arobaini katika bajeti ijayo, na kwamba wamesema wako tayari kusaidia kwa kuweka vituo vingine zaidi," alisema.

Akaongeza: "Tunataka kuweka vituo vya mafunzo kila wilaya kwa ajili ya wafugaji wa samaki ili wapate mahali pa kujifunza badala ya kwenda kwenye vituo ambavyo viko mbali."

Kuhusu uchumi wa bluu, Waziri Ndaki alisema balozi huyo alisema wanaweza kuisaidia Tanzania kupitia mpango maalum ujulikanao "Global Development Program" unaolenga kusaidia nchi zinazoendelea kwenye masuala ya uchumi wa bluu na kuiomba wizara iangalie maeneo inayoweza kunufaika kupitia mpango huo.

Aidha, Balozi Verheu alisifu Zanzibar kwa hatua ilizofikia kuhusu uchumi wa bluu na Ndaki alimhakikishia kuwa, Tanzania Bara pia imeweka malengo ya kutengeneza uchumi unaotokana na Bahari ya Hindi, maziwa, na mabwawa.


Katika sekta ya mifugo, Balozi Verheu alionesha utayari nchi hiyo kushirikiana na Tanzania kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa pande zote mbili.

Ndaki alisema Uholanzi iko tayari kusaidia maeneo ya malisho ya mifugo na ushirikiano wa kitaalamu kwa kutoa utaalamu kwa Watanzania.

"Nchi ya Uholanzi wameendelea sana katika tasnia ya maziwa na wamesema wako tayari kushirikiana na Tanzania katika kukuza soko la maziwa na wazalishaji wa maziwa ambapo hawako rasmi takriban asilimia 98, tunaweza kuwafanya hao wazalishaji wakawa rasmi na maziwa yao yakasaidia nchi kimaendeleo," alisema Ndaki

Scanned with CamScanner

TANZANITE UK 2.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mashimba Ndaki akiwa kwenye mazungumzo na Balozi wa Uholanzi nchini Tanzania Jeroen Verheu katika ofisi ndogo za Wizara ya Mifugo na Uvuvi zilizopo jijini Dar es salaam, ambapo balozi huyo amemhakikishia Waziri Ndaki nchi yake inaunga mkono mkakati wa wizara kujenga vituo vya mafunzo ya ufugaji samaki kila wilaya. Na Mpigapicha Wetu.

W
za

NA

WA
Uc
Le
ar
Ta
W
sl
k
u

Scanned with CamScanner

# Wavuvi wakwama soko la nje bidhaa za uvuvi

Na Pendo Thomas, KIGOMA

WAFANYABIASHARA wa mazao ya uvuvi katika mwalo wa Katonga na Kibirizi Manispaa ya Kigoma kwenda nchi jirani kama Congo, Burundi na Rwanda wamelalamikia biashara hiyo kufanya vibaya tangu mwaka 2020.

Wafanyabiashara hao wakizungumza na Nipashe juu ya mwenendo wa kibiashara, wamesema kwa kipindi kirefu hali imekuwa mbaya na kuwafanya wakose mitaji na baadhi yao kushindwa kurejesha madeni waliyokopa ili kukuza biashara zao.

Hamza Juma, mfanyabiashara katika Mwalo wa Katonga, alisema hali ilianza kusuasua tangu mwaka jana kipindi cha mlipuko wa ugonjwa wa Corona wakati ambapo nchi zilibadilisha utaratibu wa kuingia na kutoka ikiwamo watu kuwekewa karantini kwa siku 14.

Alieleza tangu kipindi hicho hadi sasa soko la nje sio la kueleweka tena, kutokana na baadhi ya nchi kama Burundi kuwa na masharti ya kujikinga na janga la ugonjwa wa Corona, ambayo si rafiki kwa mwingiliano wa kibiashara.

Mwenyekiti wa chama cha wavuvi Mkoa wa Kigoma, Fransis John, akielezea kwa ujumla hali hiyo alisema wengi wa watu wanaotegemea biashara ya mazao ya uvuvi kwenda nje kwa sasa hawana mitaji tena kutokana na kuzorota kwa biashara hiyo, na kuiomba serikali kutafuta namna ya kuwasaidia.

Kwa upande wake Ofisa Biashara Kigoma Manispaa, Josephat Ngomale, alisema wafanyabiashara hao wanapaswa kuwa wavumilivu hadi hali itakapo kuwa shwari pia katika nchi jirani ambazo wanazitegemea katika soko la biashara hiyo.

Alisema ni vyema wakati wakiendelea kusubiri hali kurudi kama awali kabla ya mlipuko wa ugonjwa wa Corona waelekeze nguvu kwenye kukuza soko la ndani ya nchi kwani dagaa na samaki zinazovuliwa katika Ziwa Tanganyika zinahitajika zaidi nchini katika mikoa mbalimbali .

"Nawashauri wafikie mikoa mingi zaidi ikiwamo Mbeya, Arusha na sehemu zingine zenye uhitaji badala ya kuendelea kushindwa kufanyabiashara kwa kutegemea soko la nje," alisema.

Mwalo wa Kibirizi na Katonga kwa mujibu wa taarifa kutoka kitengo cha biashara katika manispaa hiyo kwa mwaka inavua mazao ya uvuvi kiasi cha tani 630 hadi 665.

Scanned with CamScanner

MAJIRA UK 8.

# Wizara kujenga vituo vya mafunzo ya ufugaji samaki

Na Edward Kondela

BALOZI wa Uholanzi nchini Tanzania Jeroen Verheu amesema nchi yake iko tayari kusaidia ujenzi wa vituo vya mafunzo ya ufugaji samaki nchini ili kuunga mkono mkakati wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhakikisha inafikisha huduma za mafunzo hayo kila wilaya.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mashimba Ndaki akizungumza jana mara baada ya kufanya mazungumzo na balozi huyo katika ofisi ndogo za wizara zilizopo jijini Dar es Salaam, alisema Balozi Verheuameridhishwa na mkakati wa wizara ambapo katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22 imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo arobaini vya mafunzo ya ufugaji samaki.

"Sisi kama wizara tumeanza na mkakati huo na tumetenga fedha kwa ajili ya vituo arobaini katika bajeti ijayo na kwamba wamesema wako tayari kusaidia kwa kuweka vituo vingine zaidi, tunataka kuweka vituo vya mafunzo kila wilaya kwa ajili ya wafugaji wa samaki wapate mahali pa kujifunza badala ya kwenda kwenye vituo ambavyo viko mbali." alisema Ndaki.

Kuhusu uchumi wa bluu Waziri Ndaki amesema balozi huyo amemhakikishia wanaweza kuisaidia Tanzania kupitia mpango wao maalum ujulikanao "Global Development Program" ambao unalenga kusaidia nchi zinazoendelea kwenye masuala ya uchumi wa bluu na kuiomba wizara iangalie maeneo ambayo inaweza kunufaika kupitia mpango huo.

Aidha, Balozi Verheu ameisifia Zanzibar kwa hatua ilizofikia kuhusu uchumi wa bluu, huku Waziri Ndaki akimhakikishia pia Tanzania Bara imeweka malengo ya kutengeneza uchumi unaotokana na Bahari ya Hindi, maziwa na mabwawa.

Pia, katika Sekta ya Mifugo Balozi wa Uholanzi nchini Tanzania Jeroen Verheu ameonesha nia yake kubwa namna nchi yake iko tayari kuendelea kushirikiana na Tanzania kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa pande zote mbili.

Waziri Ndaki amefafanua kuwa Uholanzi iko tayari kusaidia maeneo ya malisho ya mifugo pamoja na ushirikiano wa kitaalamu kwa kutoa utaalamu kwa watanzania nao kupata utaalamu kutoka kwa watanzania juu ya sekta ya mifugo.

"Nchi ya Uholanzi wameendelea sana katika tasnia ya maziwa na wamesema wako tayari kushirikiana na Tanzania katika kukuza soko la maziwa na wazalishaji wa maziwa ambapo hawako rasmi takriban asilimia 98, tunaweza kuwafanya hao wazalishaji wakawa rasmi na maziwa yao yakasaidia nchi kimaendeleo." alifafanua Ndaki.

Katika mazungumzo hayo Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mashimba Ndaki na Balozi wa Uholanzi nchini Tanzania Jeroen Verheu wamekubaliana kuongeza wigo zaidi wa ushirikiano katika sekta za mifugo na uvuvi.



**Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mashimba Ndaki akiwa kwenye mazungumzo na Balozi wa Uholanzi nchini Tanzania Jeroen Verheu katika ofisi ndogo za Wizara ya Mifugo na Uvuvi zilizopo jijini Dar es Salaam, ambapo balozi huyo amemhakikishia Waziri Ndaki nchi yake inaunga mkono mkakati wa wizara kujenga vituo vya mafunzo ya ufugaji samaki kila wilaya.** (Picha na Edward Kondela)

Scanned with CamScanner

Yoweri Kaguta Museveni wa Uganda katika Ikulu ya Entebbe baada ya hafla ya usekwaji saini wa mkataba wa ujenzi wa Bomba la Mafuta






Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Samia Suluhu Hassan akiweka saini kwenye kitabu cha tamko la pamoja la yeye na mwenyeji wake Rais Yoweri Kaguta Museveni wa Uganda katika Ikulu ya Entebbe baada ya hafla ya usekwaji saini wa mkataba wa ujenzi wa Bomba la Mafuta

# Wizara kujenga vituo 40 vya mafunzo ya ufugaji Samaki, Uholanzi yavutiwa

Scanned with CamScanner

# Wizara kujenga vituo 40 vya mafunzo ya ufugaji Samaki, Uholanzi yavutiwa

NA MWANDISHI WETU

BALOZI wa Uholanzi nchini Tanzania Jeroen Verheu amesema nchi yake iko tayari kusaidia ujenzi wa vituo vya mafunzo ya ufugaji samaki

nchini ili kuunga mkono mkakati wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhakikisha inafikisha huduma za mafunzo hayo kila Wilaya.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mashimba Ndaki akizungumza juzi, mara baada ya kufanya mazungumzo na balozi huyo katika ofisi ndogo za Wizara zilizopo jijini Dar es Salaam, alisema

Balozi Verheu ameridhishwa na mkakati wa wizara ambapo katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22 imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo

arobaini vya mafunzo ya ufugaji samaki.

"Sisi kama wizara tumeanza na mkakati huo na tumetenga fedha kwa ajili ya vituo arobaini katika bajeti ijayo na kwamba wamesema wako tayari

kusaidia kwa kuweka vituo vingine zaidi, tunataka kuweka vituo vya mafunzo kila wilaya kwa ajili ya wafugaji wa samaki wapate mahali pa

kujifunza badala ya kwenda kwenye vituo ambavyo viko mbali." Alisema Ndaki.

Kuhusu uchumi wa bluu Waziri Ndaki alisema balozi huyo amemhakikishia wanaweza kuisaidia Tanzania kupitia mpango wao maalum ujulikanao "Global Development Program" ambao unalenga kusaidia nchi zinazoendelea kwenye masuala ya uchumi wa bluu na kuiomba wizara

iangalie maeneo ambayo inaweza kunufaika kupitia mpango huo.

Aidha, Balozi Verheu ameisifia Zanzibar kwa hatua ilizofikia kuhusu uchumi wa bluu, huku Waziri Ndaki akimhakikishia pia Tanzania Bara imeweka malengo ya kutengeneza uchumi unaotokana na Bahari ya Hindi, maziwa na mabwawa.

Scanned with CamScanner

# Uholanzi yatangaza neema kwa wafugaji samaki nchini

Na MWANDISHI WETU

BALOZI wa Uholanzi nchini, Jeroen Verheu, amesema nchi yake iko tayari kusaidia ujenzi wa vituo vya mafunzo ya ufugaji samaki, ili kuunga mkono mkakati wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kuhakikisha inafikisha huduma za mafunzo hayo kila wilaya.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki iliyopita, baada ya kufanya mazungumzo na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, katika ofisi ndogo za wizara hiyo, zilizopo jijini Dar es Salaam.

Hatua hiyo, inatokana na Balozi Verheu, kuridhishwa na na mkakati wa wizara hiyo, ambapo katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22, imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo 40, vya mafunzo ya ufugaji samaki.

"Sisi kama wizara, tumeanza na mkakati huo na tumetenga fedha kwa ajili ya vituo 40, katika bajeti ijayo na wamesema wako tayari kusaidia kwa kuweka vituo vingine zaidi.

"Tunataka kuweka vituo vya mafunzo kila wilaya, kwa ajili ya wafugaji wa samaki ili wapate mahali pa kujifunza badala ya kwenda kwenye vituo ambavyo viko mbali," ,alisema Waziri Ndaki.

Kuhusu uchumi wa bluu, Waziri Ndaki alisema balozi huyo amemhakikishia wanaweza kusaidia Tanzania kupitia mpango

> **Sisi kama wizara, tumeanza na mkakati huo na tumetenga fedha kwa ajili ya vituo 40, katika bajeti ijayo na wamesema wako tayari kusaidia kwa kuweka vituo vingine zaidi.**
>
> Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki

wao maalumu ujulikanao 'Global Development Programe', ambao unalenga kusaidia nchi zinazoendelea kwenye masuala ya uchumi wa bluu na kuomba wizara iangalie maeneo inayoweza kunufaika kupitia mpango huo.

Balozi Verheu, alipongeza Zanzibar kwa hatua iliyofikia kuhusu uchumi wa bluu, huku Waziri Ndaki, akimhakikishia pia kuwa, Tanzania Bara imeweka malengo ya kutengeneza uchumi unaotokana na Bahari ya Hindi, maziwa na mabwawa.

Balozi Verheu, pia alionesha namna nchi yake ilivyo tayari kuendelea kushirikiana na Tanzania, kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa pande zote mbili.

Katika mazungumzo hayo, Waziri Ndaki na Balozi Verheu, walikubaliana kuongeza wigo zaidi wa ushirikiano katika sekta za mifugo na uvuvi.

Scanned with CamScanner

# Balozi wa Uholanzi nchini aahidi kusaidia Tanzania ufugaji wa samaki

NA EDWARD KONDELA

BALOZI wa Uholanzi nchini Tanzania, Jeroen Verheu amesema nchi yake iko tayari kusaidia ujenzi wa vituo vya mafunzo ya ufugaji samaki nchini ili kuunga mkono mkakati wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhakikisha inafikisha huduma za mafunzo hayo kila wilaya.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi , Mashimba Ndaki akizungumza jana baada ya kufanya mazungumzo na balozi huyo katika ofisi ndogo za wizara zilizopo jijini Dar es Salaam, amesema Mhe. Balozi Verheu ameridhishwa na mkakati wa wizara ambapo katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22 imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo arobaini vya mafunzo ya ufugaji samaki.

"Sisi kama wizara tumeanza na mkakati huo na tumetenga fedha kwa ajili ya vituo arobaini katika bajeti ijayo na kwamba wamesema wako tayari kusaidia kwa kuweka vituo vingine zaidi, tunataka kuweka vituo vya mafunzo kila wilaya kwa ajili ya wafugaji wa samaki wapate mahali pa kujifunza badala ya kwenda kwenye vituo ambavyo viko mbali," alisema Waziri Ndaki.

Kuhusu uchumi wa bluu Waziri Ndaki amesema balozi huyo amemhakikishia wanaweza kusaidia Tanzania kupitia mpango wao maalum ujulikanao "Global Development Program" ambao unalenga kusaidia nchi zinazoendelea kwenye masuala ya uchumi wa bluu na kuiomba wizara iangalie maeneo ambayo inaweza kunufaika kupitia mpango huo.

Aidha, Balozi Verheu ameisifia Zanzibar kwa hatua ilizofikia kuhusu uchumi wa bluu, huku Waziri Ndaki akimhakikishia pia Tanzania Bara imeweka malengo ya kutengeneza uchumi unaotokana na Bahari ya Hindi, maziwa na mabwawa.

Pia, katika Sekta ya Mifugo Balozi wa Uholanzi nchini Tanzania Mhe. Jeroen Verheu ameonesha nia yake kubwa namna nchi yake iko tayari kuendelea kushirikiana na Tanzania kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa pande zote mbili.

Waziri Ndaki amefafanua kuwa Uholanzi iko tayari kusaidia maeneo ya malisho ya mifugo pamoja na ushirikiano wa kitaalamu kwa kutoa utaalamu kwa watanzania nao kupata utaalamu kutoka kwa watanzania juu ya sekta ya mifugo.

"Nchi ya Uholanzi wameendelea sana katika tasnia ya maziwa na wamesema wako tayari kushirikiana na Tanzania katika kukuza soko la maziwa na wazalishaji wa maziwa ambapo hawako rasmi takriban asilimia 98, tunaweza kuwafanya hao wazalishaji wakawa rasmi na maziwa yao yakasaidia nchi kimaendeleo," alifafanua Waziri Ndaki.

Katika mazungumzo hayo Waziri wa Mifugo na Uvuvi , Mashimba Ndaki na Balozi wa Uholanzi nchini Tanzania, Jeroen Verheu wamekubaliana kuongeza wigo zaidi wa ushirikiano katika sekta za mifugo na uvuvi.

Scanned with CamScanner

Mitandao @JAMVILAHABARI Jamvi la habari jamvihabari +255676807684 Email: jamvilahabari@gmail.com

GAZETI LAKO

# JAMVI LA HABARI

ISSN:Toleo Na. 2683-6548 Toleo Na. 1334 JUMATATU APRILI 12, 2021 Bei Tsh. 1000 Kenya Ksh. 60 www.jamvilahabari.co.tz

# RAIS SAMIA SULUHU, MUSEVEN WATETA

- Kwa pamoja watia saini mikataba ya kuikamilisha bomba la mafuta kutoka Uganda hadi Tanzania
- Wasema ushirikiano wao utasaidia ukuaji wa uchumi Afrika Mashariki kupitia boba hilo lenye urefu wa kilomita 1,445
- Bomba litakapokamilika litazalisha ajira 10,000 na kuwa na uwezo wa kusafirisha mapipa bilioni 6.5

UK. 4



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Samia Suluhu Hassan akiweka saini kwenye kitabu cha wageni [illegible] Rais Yoweri Kaguta Museveni wa Uganda katika Ikulu ya Entebbe [illegible]

## Balozi wa Uholanzi nchini aahidi kusaidia Tanzania ufugaji wa samaki

UK. 4

## B[illegible] 12.6/- za[illegible]mika ujenzi Da[illegible]ja la Magara m[illegible]ani Manyara

UK. 5



Scanned with CamScanner